

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**  
**MKOA WA KATAVI**

Anwani ya Simu: "AFYA", KATAVI  
Simu ya Mdomo: 025-252957128  
Fax No. 025- 252957129



Hospitali ya Rufaa Mkoa,  
S. L. P. 449,  
**KATAVI**

**MKATABA WA SAMANI HOSPITALI YA RUFAA KATAVI**

**Mkataba na ME.007/KTVRRH/2021/2022/G/04**

Mkataba huu umefikiwa leo hii tarehe 05. mwezi 01... Mwaka 2022 hapa Mpanda, **KATI YA MKURUGENZI WA HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA KATAVI** (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MWAJIRI**) kwa upande mmoja na MFUNA MSAMBA (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **Mtoa huduma ya Samani (Furniture)**, Mwajiriwa kwa upande mwingine).

**Kwakuwa**, Mwajiri anahitaji mtoa huduma ya Samani za chumba cha telemedicine kwa ya Tsh. 9,000,000 (Milioni tisa) bila VAT.

**Na kwakuwa**, Mtoa huduma ya Samani anao ujuzi, uwezo na uzoefu wa kutoa huduma kwa taasisi za Serikari na ana nia ya kutekeleza kazi tajwa **Hivyo basi**, Mwajiri na Mwajiriwa wanakubaliana yafuatayo;

1. Kwamba, malipo kwa mwajiriwa yatafanywa na mwajiri mara baada ya mtoa huduma ya Samani kutoa huduma hiyo kwa ukamilifu na baada ya kukaguliwa na kukubaliana na mwajiri
2. Endapo mwajiriwa atatoa Samani zisizo na ubora au visivyozingatia ubora au visivyozingatia vigezo/viwango vya mwajiri (specifications) atatakiwa kurudisha vifaa hivyo na kuleta vifaa vyenye ubora unaohitajika kwa gharama zake kwa wakati
3. Kwamba, hakutakuwa na malipo ya awalikatika mkataba huu.
4. Kwamba, mwajiri atasaini nyaraka za kukiri mapokezi ya Samani baada ya vifaa kukaguliwa na kamati ya mapokezi, kukidhi mahitaji.
5. Kwamba, mwajiriwa atatoa huduma ya Samani ndani ya siku 14 tangu tarehe aliyopokea mahitaji toka kwa Mwanjiri.
6. Kwamba, upande wowote unaweza kuvunja mkataba huu kwa notisi ya maandishi ya siku 7 ya kusudio la kuvunja mkataba kwa upande mwingine ikiwa upande mwingine utashindwa kutekeleza masharti ya Mkataba huu
7. Kwamba, ikitokea upende wowote haujatekeleza wajibu wake ipasavyo, pande zote mbili zitakutana ndani ya siku (2) ili kuona namna bora ya upande ambao haujatekeleza wajibu na kutekeleza wajibu huo ipasavyo.

8. Kwamba, mwajiriwa atawasilisha nyaraka za madai ya huduma ya vifaa alizotoa baada ya vifaa kukaguliwa na kupokelewa na mwajiri na kwamba hakuna malipo yatakayofanywa kwa mwajiriwa bila kuwasilisha nyaraka za madai.
9. Kwamba, jukumu la usalama na usafirishaji wa huduma ya vifaa vinavyonunuliwa itakuwa ni la mwajiriwa mpaka pale vifaa hivyo vitakapofika eneo husika na kupokelewa na mwajiri.
10. Kwa kuwa mkataba huu umeingiwa kwa nia njema na kwa manufaa ya pande mbili, iwapo kutatokea mgogoro au kutokuelewana kokote katika utekelezaji wa mkataba huu basi MSULUHISHI anayekubalika na upande zote atatafutwa ili kusuluhisha mgogoro huo. iwapo muafaka hautapatikana basi suala hilo litapelekwa mahakamani.
11. Kwamba mkataba huu unatawaliwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  
MKATABA huu umetiwa saini leo na hawa wafuatao;

**MWAJIRI**

JINA: JUSTINA ADJUMIRWA  
 CHEO: NOKU  
 ANWANI: 449  
 SAHIHI: [Signature]

TAREHE: 5/01/2022  
 NGANGA MFAWIDHI  
 HOSPITALI YA RUFAA  
 S. L. P. 216  
 KATAVI

**MBELE YA**

JINA: ZAWAD P. Mwanasa  
 CHEO: HRD  
 ANWANI: 449  
 SAHIHI: [Signature]

TAREHE: 5/01/2022

**MTOA HUDUMA**

JINA: MFUNA MSAMBA  
 CHEO: DIRECTOR  
 ANWANI: 216  
 SAHIHI: [Signature]

**MBELE YA**

JINA: JOHN GASPAR  
 CHEO: MANAGER  
 ANWANI: 216  
 SAHIHI: J.G

INVESTMENT LIMITED  
 P.O. BOX 216  
 KATAVI  
 TAREHE: 05/01/2022  
 TAREHE: 05/01/2022